# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1033

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-770-8

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI SANAA NA MICHEZO STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

# 2023

Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 1 19/10/2024 14:41

©Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-770-8

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa Somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 2 19/10/2024 14:41

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali....................iv
Vifupisho ....................v
Shukurani ....................vi
1.0 Utangulizi....................1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu....................1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ....................2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu....................2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sanaa na Michezo ....................3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji....................3
6.1 Mkufunzi....................4
6.2 Mwalimu Tarajali....................4
6.3 Mzazi/mlezi....................4
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji....................5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ....................5
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ....................5
10.0 Idadi ya Vipindi....................6
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji....................6
Bibliografia ....................25

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Mwalimu Tarajali ........ 3

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa alama za upimaji endelevu ........ 6

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza........ 7

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili ........ 18

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo ni somo la lazima katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Lengo la kufundisha somo hili ni kumwezesha mwalimu tarajali kuwa na umahiri katika utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi, kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo katika Elimu ya Msingi. Vilevile, somo hili litamwezesha mwanafunzi kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maigizo, uimbaji na upigaji wa ala za muziki, uchoraji, ufinyanzi, matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji mazoezi ya viungo, na michezo

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mkufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Aidha, Muhtasari utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi tarajali stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 1 19/10/2024 14:41

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, st adi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya elimu ya ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali wa wanafunzi wenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla umejikita katika misingi ya kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijiti na uzalendo ambao umefafanuliwa katika maeneo ya ujifunzaji na masomo kama ifuatavyo:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;

(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;

(e) Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 2 19/10/2024 14:41

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (instructional leadership);

(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based action research*).

## 5.0 Umahiri mkuu na umahiri mahususi wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sanaa na Michezo

Jedwali lifuatalo linaonesha umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Mwalimu Tarajali*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji<br>1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uimbaji na upigaji wa ala za muziki<br>1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji<br>1.4 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo |
| | 1.5 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo<br>1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi<br>1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi |
| 2.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa na mashindano ya michezo | 2.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa<br>2.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi hii ya Elimu unategemea ushirikiano baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi katika kutimiza wajibu wao ambao ni:



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 3 19/10/2024 14:41

**6.1 Mkufunzi**

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

**6.2 Mwalimu Tarajali**

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini wanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

**6.3 Mzazi/mlezi**

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 4 19/10/2024 14:41

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo utaongozwa na ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo zinazomshirikisha mwalimu tarajali katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, changamoto za ulemavu na mahitaji ya ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinavyokidhi mahitaji, umri, na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha kwamba mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia, kushika zana na kuzitumia. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Vilevile, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa ziandaliwe kwa kuzingatia usawa wa jinsia na ujumuishi. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizopendekezwa ni pamoja na kompyuta, printa, tableti, sidii, manila, bangokitita, matini mbalimbali, picha zisizo na ubaguzi wa kijinsia, kinasa-sauti, televisheni, redio, kamusi, na kadi za alama. Zana hizi zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sanaa na Michezo utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Elimu ya Stashahada Elimu ya Msingi. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali katika kumudu misingi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi na kutumia matokeo ya upimaji kutathmini maendeleo ya mwalimu tarajali. Upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali uzingatie usawa wa kijinsia na ujumuisho. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana zinazotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, shajara, kazimradi, uwasilishaji darasani na mitihani ya mwisho wa  muhula. Vilevile, tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali ni muhimu kufanyika ili kubaini ni kwa kiasi gani anajenga umahiri uliokusudiwa. Matokeo ya tathmini yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya elimu ya ualimu yanafanikiwa.



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 5 19/10/2024 14:41

Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha asilimia hamsini (50%), mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli ya Upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mitihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mitihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mitihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi vitano (5) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana za kufundishia na kujifunzia na idadi ya vipindi. Jedwali lifuatalo linaonesha maudhui yanayopaswa kufundishwa katika Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sanaa na Michezo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 6 19/10/2024 14:41

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji zimechambuliwa kwa ufasaha | Maleba, ngoma, filimbi, vifaa vya kuigizia, projekta, matini, bangokitita, kalamu rashasha | 33 |
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, radio, video, kipaza sauti, gitaa, kinasa sauti, ngoma, marimba, bangokitita, chati pindu, kalamu rashasha, matini | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji yamefafanuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, maunzi, simujanja, printa, laini ya kompyuta, kamera, *memory card* | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, kamera, *memory card* | |
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji katika darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Maleba, ngoma, filimbi, vifaa vya kuigizia, projekta, matini, bangokitita, kalamu rashasha | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji nje ya darasa | Mbinu za kuratibu shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji nje ya darasa zimechanganuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, gundi ya karatasi, vipaza sauti, vinasa sauti, makunzi mbalimbali | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uimbaji na upigaji wa ala za muziki | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki zimechambuliwa kwa ufasaha | Kinanda, gitaa, ngoma, radio, marimba, bangokitita, kalamu rashasha, matini, manyanga, tarumbeta, filimbi, kinasa sauti, kompyuta yenye maunzi laini ya muziki, kipaza sauti, projekta, matini mbalimbali | 31 |
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji uimbaji na upigaji ala za muziki zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, radio, video, kipaza sauti, gitaa, kinasa sauti, ngoma, marimba, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, matini mbalimbali | |



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 9 19/10/2024 14:41

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa uimbaji na upigaji ala za muziki yamefafanuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, maunzi laini ya kompyuta, *pitch pipe,* ala za muziki | |
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uimbaji na upigaji ala za muziki zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, kamera, kipaza sauti, kinasa sauti, ala za muziki | |
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki katika darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vipaza sauti, vinasa sauti, makunzi mbalimbali, ala za muziki | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki nje ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa kuimba na kupiga ala za muziki nje ya darasa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vipaza sauti, vinasa sauti, makunzi mbalimbali, ala za muziki | |
| | 1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji zimechambuliwa kwa ufasaha | Rangi za maji, brashi, karatasi nyeupe, maji, paleti, kalamu ya risasi, bangokitita, chatipindu, kalamu rashaha, vichongeo, rula, gundi ya karatasi, gundi ya maji, malapulapu safi ya nguo, mfutio, kompyuta, projekta, vipande vya sponji. | 41 |



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 11 19/10/2024 14:41

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji zimechambuliwa kwa ufasaha | Rangi za maji, brashi, karatasi, maji, paleti, kalamu ya risasi, bangokitita, chatipindu, kalamu rashaha, kompyuta, projekta, simujanja, radio, video, kipaza sauti, kinasa sauti, kamera, matini mbalimbali, karatasi nyeupe | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji wa picha | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji wa picha yamefanyika kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, maunzi laini ya kompyuta, kamera, saa, *memory card* | |
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji wa picha zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, kamera, saa, karatasi nyeupe | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji kwa darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, makunzi | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji nje ya darasa | Mbinu za kuratibu shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji wa picha nje ya darasa zimechanganuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, makunzi | |
| | 1.4 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo (*kuimarisha afya, utimamu wa mwili na stadi za michezo*) | Matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo yamechambuliwa kwa ufasaha | Matini mbalimbali, bangokitita, chatipindu kalamu rashasha, mipira, filimbi, chati za aina mbalimbali ya mazoezi, kamba za mazoezi, futi kamba, projekta, DVDs, vifaa vya kupimia sukari, mafuta, uzito na urefu, eneo la kufanyia mazoezi | 33 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo | Mbinu za uchopekaji wa maswala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo yamechambuliwa kwa ufasaha | Bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, projekta, vifaa husika vya mazoezi ya viungo. | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo yamefafanuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, maunzi laini ya kompyuta, kamera, saa, radio | |
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, kamera, saa, maunzi laini ya kompyuta, radio, Vifaa vya mazoezi ya viungo, Vifaa vya kupima sukari, shinikizo la damu, mafuta, urefu | |



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 14 19/10/2024 14:41

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo (*kuimarisha afya, utimamu wa mwili na stadi za michezo*) katika darasa kubwa | Matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo kwa darasa kubwa yamechambuliwa kwa ufasaha | Matini mbalimbali, bangokitita, chatipindu kalamu rashasha, mipira, filimbi, chati za aina mbalimbali ya mazoezi, kamba za mazoezi, futi kamba, projekta, DVDs, vifaa vya kupimia sukari, mafuta, uzito na urefu, eneo la kufanyia mazoezi | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo nje ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo nje ya darasa zimechanganuliwa kwa ufasaha | Vifaa husika vya mazoezi ya viungo, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu, saa ya michezo | |
| | 1.5 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo | Matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo yamechambuliwa kwa ufasaha | Matini mbalimbali, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, mipira, filimbi, chati za aina mbalimbali ya mazoezi, kamba za | 37 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mazoezi, futi kamba, projekta, DVDs, vifaa vya kupimia sukari, mafuta, uzito na urefu, eneo la kuchezea, mikeka, vibao, vikwazo vya jimnastiki, bastola/ vibao vya riadha, saa ya michezo, vibendera, ubao wa matokeo | |
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo | Mbinu za uchopekaji wa maswala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo yamechambuliwa kwa ufasaha | Bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, projekta, vifaa vya michezo husika, vifaa vya kupimia sukari, uzito, shinikizo la damu, urefu na mafuta | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo yamefafanuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, maunzi laini ya kompyuta kamera, saa, radio, vifaa vya michezo husika, vifaa vyakupimia sukari, | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | shinikizo la damu, mafuta, urefu na uzito | |
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa michezo zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, kamera, saa, maunzi ya kompyuta, radio, Vifaa vya mazoezi ya viungo vifaa vya kupimia sukari, shinikizo la damu, mafuta, urefu | |
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo katika darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vifaa vya michezo husika, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo nje ya darasa | Mbinu za kuratibu shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo nje ya darasa zimechanganuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vifaa vya michezo husika, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu | |

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo katika Elimu ya Msingi | 1.6 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi zimechambuliwa kwa ufasaha | Projekta, matini, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha | 47 |
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, kamera, | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi yamechanganuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, gundi ya karatasi, vipaza sauti, makunzi mbalimbali | |
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vifaa vya michezo husika, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu | |



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 18 19/10/2024 14:41

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi katika darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vifaa vya michezo husika, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi nje ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi nje ya darasa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vifaa vya michezo husika, daftari la kutunza kumbukumbu, kalamu | |
| | 1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi | (a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi zimechambuliwa kwa ufasaha | Kinanda, gitaa, ngoma, radio, marimba, bangokitita, kalamu rashasha, matini, manyanga, tarumbeta, filimbi, kinasa sauti, kompyuta yenye maunzi laini ya muziki, kipaza sauti, projekta, matini mbalimbali | 48 |



Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 19 19/10/2024 14:41

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi zimechanganuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, maunzi laini ya kompyuta, *pitch pipe* | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi | Matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi yamezingatiwa | Kompyuta, projekta, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, vipaza sauti, vinasa sauti, makunzi mbalimbali | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi zimetumika vema | Udongo wa mfinyanzi, maji, visu, gurudumu la mfinyanzi, kalamu rashasha, bangokitita, chatipindu, gundi ya karatasi, vyombo vya maji safi, nyuzi za nailoni au waya, makaratasi ya nailoni, marapurapu safi ya nguo | |
| | | (e) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi katika darasa kubwa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi katika darasa kubwa zimechambuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, radio, video, kamera, saa, kipaza sauti, bangokitita, chatipindu, kalamu rashasha, matini, udongo wa mfinyanzi, gurudumu la mfinyanzi | |
| | | (f) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi nje ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi nje zimefafanuliwa kwa ufasaha | Kompyuta, projekta, simujanja, printa, kamera, saa, gundi ya mbao | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa na mashindano ya michezo | 2.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa | a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya darasa zimechambuliwa kwa ufasaha | Projekta, printa kompyuta,vipasa sauti,video, ngoma, bango kitita, maleba, rangiza mafuta, kalamu rashasha, simu janja, kamera, chati pindu, kisana sauti,kipaza sauti | 40 |
| | | b) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya shule | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya shule zimechambuliwa kwa ufasaha | Projekta, printa kompyuta,vipasa sauti, video, ngoma, bango kitita, maleba,rangiza mafuta, kalamu rashasha, simu janja, kamera, chati pindu, kisana sauti, kipaza sauti na eneo la kufanyia maonesho. | |
| | | c) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya jamii | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya jamii zimechambuliwa kwa ufasaha | Projekta, printa kompyuta, vipasa sauti, video, ngoma, bango kitita, maleba,rangiza mafuta, kalamu rashasha, simu janja, kamera, chati pindu, kisana sauti, | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kipaza sauti, eneo la kufanyia maonesho na makunzi. | |
| | | d) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa kitaifa na kimataifa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa ngazi ya kitaifa na kimataifa zimechambuliwa kwa ufasaha | Projekta, printa kompyuta,vipasa sauti,video, ngoma, bango kitita, maleba, rangiza mafuta, kalamu rashasha,simu janja, kamera, chati pindu, kisana sauti, kipaza sauti, eneo la kufanyia maonesho na simujanja | |
| | 2.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo | a) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya darasa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya darasa zimechambuliwa kwa ufasaha | Mipira, filimbi, vibendela, chatipindu, kompyuta, projekta, radio, video, kinasa sauti, kipaza sauti, vifaa vya kupimia sukari na kamera. | 40 |
| | | b) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya shule | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya shule zimechambuliwa kwa ufasaha | Mipira, filimbi, vibendela, chatipindu, kompyuta, projekta, radio, video, kinasa sauti, kipaza sauti, vifaa vya kupimia sukari na kamera. | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za kutendwa | Vigezo vya upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | c) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya mihezo ngazi ya jamii | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya jamii zimechambuliwa kwa ufasaha | Mipira, filimbi, vibendela, chatipindu, kompyuta, projekta, radio, video, kinasa sauti, kipaza sauti, vifaa vya kupimia sukari na kamera. | |
| | | d) Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya kitaifa na kimataifa | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo ngazi ya kitaifa na kimataifa zimechambuliwa kwa ufasaha | Daftari la kutunza kumbukumbu, koni,bips, Mipira, filimbi, vibendela, chatipindu, kompyuta, projekta, radio, video, kinasa sauti, kipaza sauti, vifaa vya kupimia sukari na kamera. | |

## Bibliografia


Europe, S. (2019). *Music Syllabus - Primary Circle.* Europa: Office of the Secretary-General.

Europaea, S. (2019). *Music Syllabus - Primary Circle.* Europa: Office of Secretary General.

Isembwa I.P. & Biman M.S (2008). *Stadi za Kazi Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne.* Educational Book Publisher.

Jarret, S., & Day, H. (2008). *Music Composition for Dummies.* Canada: Wiley Publishing.

Milller, M. (2005). *Music Theory 2nd Ed.* Penguine Group - Inc. 375 Hudson Street.

Mohanna, K., Chambers, R., & Wall, D. (2007). Developing your teaching style: increasing effectiveness in healthcare teaching. *Postgraduate medical journal, 83*(977), 145– 147. https://doi.org/10.1136/pgmj.2006.054106

Sternberg, R. J. (1997*). Thinking Styles.* Cambridge University.

Sibuga K.K. (2011). *Stadi za Kazi Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la VII.* Educational Book Publisher.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2021). *Stadi za Kazi Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la V-VI.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* (Toleo la 3). Shanghai Kangshi Printing Co. Ltd.

Tanzania Institute of Education (2011). *Physical Education Teacher's Manual for secondary schools. FORM I-IV.* Tanzania Institute of Education.

MoEVT (2010). *Physical Education and Sports Syllabus for Advance Secondary Education Form V-VI.* Ministry of Education and Vocational Training.

MoEVT (2010). *Physical Education and Sports Syllabus for Secondary Schools Form I-IV.* Ministry of Education and Vocational Training.

MoEVT (2010). *Fine Art Syllabus for Advanced Secondary Education Form V-VI*. Dar es Salaam, Ministry of Education and Vocational Training.

MoEC: (2005). *Fine Art Syllabus for Secondary Schools. Form I-IV*. Ministry of Education and Culture.




Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Sanaa na Michezo FINAL.indd 25 19/10/2024 14:41

MoEVT (2009). *Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Elimu kwa Michezo-Ngazi ya Cheti; Michezo.* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

MoEVT (2009). *Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Elimu kwa Michezo- Ngazi ya Cheti; Somo la Ualimu*. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

MoEVT (2009). *Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Elimu kwa Michezo - Ngazi ya Cheti; Usimamizi na Usalama Katika Elimu kwa Michezo*. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.